Teacher.co.ke

**MUHULA WA KWANZA**

**KIDATO CHA TATU (3)**

**KARATASI YA TATU (102/3)**

**MUDA: SAA 2 ½**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**MAAGIZO;**

a. Swali la kwanza ni la lazima
b. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
c. Jibu jumla ya maswali manne
d. Kila swali ni alama 20
e. Tumia lugha ya Kiswahili

**SEHEMU YA A:USHAIRI**

**Swali la lazima**

**Soma shairi kisha ujibu maswali**

Angawa mdogo dagaa, amekomaa
Kaanga kidogo, atakufaa
Kalia kinaya, h'ondoa njaa

Teacher.co.ke

Wa kwako udogo, kijana sio balaa
Na sio mzigo ,kijana bado wafaa
Toka kwa mtego ,kijana sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana wacha kukaa
Chimbua mhogo, kijana Husibung'aa

Na wake udogo, dagaa hajambaa
Kuliko vigogo ,dagaa hajambaa
Hapati kipigo ,dagaa hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Sihofu magego, Kijana nawe wafaa

Kazana kidogo, kijana kugagaa

Maswali

a)Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

***Kijana /dagaa***

b)Eleza arudhi zilizofuatwa katika shairi hili (alama 4)

***Mpangilio wa beti***

***Urari wa vina katika kila ubeti***

***Urari wa mizani katika kila mshororo***

***Urari wa mishoror katika kila ubeti***

c)Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

***Lahaja –magego***

***Kuboronga sarufi-na wake mdogo-na udogo wake***

***Inkisari-wafaa -unafaa***

d)Tambua bahari katika shairi hili kwa kutegemea;

i)Vipande vya mishororo-***mathinawi-vipande viwili katika mshororo***

ii)Mpangilio wa vina -***mtiririko***

iii)Idadi ya mishororo-***tathlitha-utatu***

e)Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 3)

***Kijana nakupa nasaha kwamba ukubwa ni jaa na ni vizuri utie bidii kabisa kazini . Ni vizuri kuchimbua mihogo ili apate riziki.***

f)Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 3)

***Istiari-jikaze kimbogo***

***Msemo-kuwa taa***

***Takriri-dagaa***

***Methali –ukubwa ni jaa***

g)Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

***kuhimiza/ ya matumaini***



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**SEHEMU YA B: Riwaya ya Chozi la heri na Asumpta Matei**

2. Athari ya vita katika nchi ya Wahafidhina ni kioo cha bara ya Afrika. Jadili(alama 20)

I. ***Watu kuuawa***
II. ***Watu kuacha makwao na kukumbilia maisha yao huku kupoteza mali kwani waliokimbia makwao na kila walichokiacha kilitekelezwa***
III. ***Kupora maduka ya kihindi ,kiarabu na ya Waafrika wenzao***
IV. ***Misafara ya wakimbizi ikawa kwenye barabara na vichororo vya Wahifidhina***
V. ***Mizoga ya watu na wanyama kutapakaa ovyo***
VI. ***Magofu ya majumba yalioteketekezwa kwa moto***
VII. ***Uharibifu wa mali na mazingira***
VIII. ***Nyimbo za uchochezi kwa mpinzani wa Mwekevu zinazozua ghasia baada ya uchaguzi***
IX. ***Kuchomwa kwa magari kana kwamba ni mabiwi ya taka***
X. ***Vilio kutoka kwa waliokuwa wakiteketezwa***
XI. ***Kubakwa kwa mabinti wa Kaizari yaani Lemi na Mwanaheri***
XII. ***Askari wa Fanya Fujo uone kuwafyatulia risasi vijana walioamua kufa kishujaa***
XIII. ***Magonjwa ya homa ya matumbo wakiwa kambini***
XIV. ***Njaa na ukosefu wa maji kambini***
XV. ***Kukimbilia chakula kwa watu wazima jinsi wafanyavyo watoto***
***Zozote 10*2=20***

AU

3. Riwaya ya Chozi la heri imejaa aina mbalimabli za migogoro.Jadili(alama 20)

I. ***Mgogoro wa Familia ya akina Pete ambaye anaonekana hana mshabaha na babake na kupelekwa kwa bibi***
II. ***Mgogoro wa kisiasa kuna mgogoro kati ya wafuasi wa Mwekevu na wa mpinzani wake mwanamume***
III. ***Mgogoro wa kikoloni anapuuza sera za mwafrika hasa za umiliki wa ardhi na kumchukua mwafrika kama mfanyikazi wake***
IV. ***Mgogoro wa ukabila .Subira anafukuzwa na mama mke kwa sababu ya kutoka jamii tofauti.***
V. ***Ridhaa anaitwa 'mfuata mvua ' na kutengwa na wenzake waliomwita mwizi***
VI. ***Mgogoro wa nafsi yake Pete jambo linalomfanya kutumia dawa ya panya kwa lengo la kujiangamiza***
VII. ***Mgogoro wa utawala vijana-wanaamua kutotoka kwa njia jambo ambalo linasababisha kupigwa risasi na kujifia***
VIII. ***Mgogoro wa kiimani-Lily Imani yake ya Kikristo inakinzana na Imani ya Mwangeka kuwa askari***
IX. ***Mgogoro wa kiuchumi –Dick anakataa kazi ya ulanguzi wa dawa za kulevya ila anashindwa atapata vipi chakula asipokuabali kazi hii***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

X. ***Migogoro wa kisaikolojia darasani –Umu anaonekana akiwazia mambo mengi mwalimu anapomwambia arudi darasani .Aidha Mwanaheri anasema anashindwa kumsikiliza mwalimu juu ya mawazo yanayompitia akilini***

XI. ***Mgogoro wa ufisadi-watu wanapewa hati miliki ghushi.Aidha maskini ambao mashamba yao yalinyakuliwa na kuunda tume ya uchunguzi inagwa hawapati ripoti ya uchunguzi huo.***

XII. ***Mgororo wa kitamaduni-Tuuama licha ya kjua fika madhara a tohara yaliomkabili ,hospitalii anatetea utamaduni wa kupasha tohara wasichana***

XIII. ***Mgogoro wa kitabaka-matajiri wanapewa mikopo ya elimu iliotengewa watoto maskini kama alivyosema Kipanga.***

XIV. ***Mgogoro wa matibabu-Selume analalamika jinsi ambavyo viongozi katika hospitali za umma wanavyonyakuwa dawa na kuacha hospitali bila dawa.***

XV. ***Mgogoro wa ardhi-serikali inaamua kuwaondosha watu kutoka msitu wa mamba bila kuwafidia.***

***Zozote 10*2=20***

**<u>SEHEMU YA C: Hadithi ya Mapambazuko na machweo na hadithi nyingine</u>**

4.''Ondoa wasiwasi mhibaka ,***you are in very safe hands*** .Usiulize maswali , ***its okay***. Tulikuja sote jana baada ***ya dance*** , umesahau hivi?'

i)Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)

***Ni maneno ya Agelica***

***Akimwambia Tembo***

***Wakiwa kwa Angelica Majengo***

***Tembo alikuwa amelala kwa Agelica baada ya burudani usiku uliotangulia***

ii)Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo.(alama 4)

***mhibaka-lakabu***

***kuchanganya ndimi-you are in very safe hands***

iii)Jadili madhara ya pombe katika jamii kama inavyodhihirika katika hadithi ya Kila Mchezea Wembe.(alama 12)

I. ***Huleta mgogoro katika ndoa***
II. ***Kuvunjika kwa ndoa-bibi yake anapotaka talaka***
III. ***Kukusosana na jamii***
IV. ***Upofu-Tembo anapokuwa mgonjwa***
V. ***Kifo-Moshi kufa***
VI. ***Kukosa utu-Tembo hamhurumii Mama Pima anapofungwa***
VII. ***Mama Pima kufungwa kwa sababu ya uuzaji wa pombe haramu***
VIII. ***Kuingia mtegoni kwa vimada baada ya kulewa kwa anasa***

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

IX. *Kuleta ukiwa –anapokosa marafiki kuja kumwona hospitali*
X. *Kukosa kuwaajibika kama mzazi-watoto wa Tembo kukosa chakula*
XI. *Tembo kupoteza kazi*
XII. *Kuleta uzembe-Tembo anapomka kuchelewa*
XIII. *Huleta mappuza -Anaondoka bila kumjuza mkewe*
*Zozote 12*1=12*

Au

5. Eleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi ya Sabina.(alama 20)

I. *Nyaboke anapopata mimba akiwa kidato cha pili masomo yake yanakatika*
II. *Jana dume lililompa uja- uzito linamkana kumwachia Nyaboke ulezi*
III. *Nyaboke anapougua analaumiwa na jamii kupata mtoto nje ya ndoa*
IV. *Aanapokataa wanaume waliokuja kumchumbia na kuwakataa analaumiwa na jamii bado*
V. *Kukosa mtetezi – wazazi wa Sabina walipoaga na kwenda kuishi na mjombake*
VI. *Kudhulumiwa na jinsia yake-Yunuke bibi ya mjomba wake*
VII. *Kupigwa mfululizo baada ya kufika nyumbani akiwa amechelewa*
VIII. *Yunuke alipoiona barua alimshuku Sabina kuwa anatembea na wanaume na anamtukana sana*
IX. *Anachunga ng'ombe akitoka shuleni*
X. *Anatukanwa*
XI. *Anauza maziwa kila asubuhi kabla ya kwenda shuleni*
XII. *Anashtumiwa kwa kosa ambalo hajafanya-eti ameiba pesa za maziwa kwa sababu hakuonekana sokoni asubuhhi hiyo*
XIII. *Anaamrishwa na Yunuke kwenda shambani alipotoka shuleni kukitapakiza kisozo kilichoanza kunuka*
XIV. *Anakamua ng'omba na kutayarisha chajio kila siku kumwachia muda mfupi wa kudurusu*
XV. *Anakejeliwa kuwa hakuwa na akili ya kusoma ila ya kuchangamkia barua na mambo ya wanaume tu*
XVI. *Kupangiwa ndoa ya mapema baada tu ya matokeo ya mtihani*
XVII. *Kunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo hata kama angepasi vizuri kwa sababu yeye ni msichana*
XVIII. *Anaonekana kama chambo cha kunasia mali kupitia mahari ambayo yangetolewa iwapo angeozwa*
XIX. *Hapewi nafasi ya kujichaguliwa mume –anatafutiwa mwendesha pikipiki kama mume bila hiari yake*
XX. *Hahusishwi katika mipango ya ndoa yake*
Zozote 20*1=20

**SEHEMU YA YA D: <u>Tamthilia ya Bembea ya maisha na Timothy Arege</u>**

6. Tambua nafasi ya mwanamke jinsi ilivyoshughulikiwa na mwandishi katika Tamthilia hii.(alama 20)

I. *Wavumilivu-Sara anamvumilia Yona anapomtesa kwa kukosa kumpa watoto*
II. *Hatoki katika ndoa- Yona anapomsimanga Sara kwa kutompa mtoto mvulana*



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

III. *Msaidizi-Yona alipopoteza kazi yake kwa sababu ya ulevi anamsaidia kuwalipia watoto wao karo*
IV. *Sara anaposhindwa kumhudumia Yona kwa sababu ya ugonjwa anamtafuta Dina kuliziba pengo hilo*
V. *Sara anamtetea Neema kwa babake ambaye anaona hajawasidia ipasavyo*
VI. *Sera anaelewa mila na desturi ya kutolala kwa mwanawe aliyeolewa hivyo kumtetea Bunju bwanake Neema*
VII. *Neema anajumukika kuwasomesha wanuna wake hadi chuo kikuu*
VIII. *Sara anamtaka Asna aolewe kwni amefikisha amri ili awaone wajukuu wake kabla hajafa*
IX. *Sara anamkataza Asna asimsimange Bunju kwani yeye ni kama ndugu*
X. *Neema anawashughulikia wazazi wake wanapokuwa wagonjwa- kuwanunulia jiko la gesi,kuwajengea nyumba na hata kuwatafutia mfanyikazi wa kuwasaidia*
XI. *Neema anamsaidia mtoto wake kazi ya ziada ya shuleni-Lemi*
XII. *Sara anahakikisha ana mavuno ya kutosha ya mpunga kwa sababu ya familia yake*
XIII. *Sara amshauri Asna aache kuishi maisha ya ukata mjini arudi mashambani*
XIV. *Mwanamke ni kielelezo cha kupinga utamaduni uliopitwa na wakati-Asna anapopinga kuolewa eti umri umetimia*
XV. *Mwanamke katika hadithi anachangia kuibua ploti kwa njia tofauti tofauti*
XVI. *Pia amechimuza maudhui kadha wa kadha katika hadithi hii*

*Zozote 10*2=20*

AU

7. 'Ulimwengu umeendelea sana''

a) Weka dondoo katika muktadha wake. (alama 4)

*Haya ni maneno ya Sara*

*Akimwambia Neema wakiwa*

*Wakiwa nyumbani kwa kina Neema kijijini*

*Sara alikuwa ametoka hospitalini alikokuwa akitibiwa*

b) Fafanua sifa sita za msemaji.(alama 6)

I. *Mkakamavu-Sara anabakia katika ndoa yake baada ya kupitia changamoto nyingi*
II. *Mvumilivu-Anamvumila Yona alipokosa kazi kwa kulipia watoto wake karo*
III. *Mhafidhina-anamtaka Asna aolewe baada ya kufikisha umri wa kuolewa*
IV. *Ana mapenzi ya dhati kwa mumewe-anataka kurudi shamba ili amshughulikie mumewe*
V. *Ana bidii-amevuna mpunga wa kutosha kwa sababu ya familia yake*

c) Eleza kwa nini huku kwa msemaji hakujaendelea.(alama 10)

I. *Raia haijushughulishi na maendeleo-Tunasubiri nchi zingine zizalishe sisi tutumie tu-utegemezi*
II. *Raia wana hujuma za kuchimbana na kusutana badala ya kujishughulisha na maendeleo*
III. *Wengi wana maneno ya kuvuta nyuma azma ya maendeleo*
IV. *Wanaume wengi badala wajishughlishe na maendeleo wanatumia muda mwingi wakijishughulisha na ulevi*
V. *Wanatumia pesa zote katika ulevi na sio maendeleo*



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

***5*2=10***

**SEHEMU YA E: Fasihi simulizi**

8. a) Taja na ufafanue hatua zozote nne za utafiti nyanjani kwa mfuatano wake.(alama 8)

I. ***Maandalizi***
II. ***Kuteua sampuli/vifani/waelekezi/wajibu***
III. ***Kukusanya data***
IV. ***Kuhifadhi data***

b) Tambua baadhi ya changamoto ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani(alama 8)

I. ***Kukosa idhini ya kufanya utafiti kutoka uongozi wa kiserikali au wazee wa kijiji***
II. ***Usafiri***
III. ***Ukosefu wa usalama***
IV. ***Vikwazo vya mawasiliano***
V. ***Kuptisha muda wa kufanyia utafiti***
VI. ***Kushindwa kufasiri lugha kutoka lugha asilia hadi pokezi***
VII. ***Vifani kukataa kutoa maelezo wakidai kulipwa***
VIII. ***Vifani kukataa kuwasilisha vizuri wakiogopa ugeni wa mtafiti***

c) Data iliyohifadhiwa kwa njia ya maandishi inafisha vipi uhalisia wa Fasihi simulizi?(alama 4)

I. ***Kidato / kiimbo /sauti hupotea***
II. ***Ishara za mwili na miondoko haziwezi kunukuliwa kama kwa kutokea kwake***
III. ***Maleba hayataonekana***
IV. ***Mwingiliano wa moja kwa moja kati ya fanani na hadhira hupotea***
V. ***Taathira ya moja kwa mja kati ya fanani na mwasilishaji hupotea***

***Mwisho***



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes